



IOWA CITY
PUBLIC LIBRARY



BookMobile

IOWA CITY PUBLIC LIBRARY

Je, Maktaba inayohamishika (Bookmobile) ni nini?

Bookmobile ni huduma ya maktaba inayohamishika inayotolewa na Maktaba ya Umma Jijini Iowa (ICPL). Mbali na vitabu vipyä maarufu na DVD zilizo kwenye Maktaba inayohamishika, unaweza kuchukua kitu chochote kutoka ICPL kwa kukishikilia au kuomba kukichukua kwenye Maktaba inayohamishika.

Je, nitachukua vitabu vipi?

Mtu ye yote aliye na kadi ya Maktaba ya ICPL anaweza kuchukua vitu kutoka kwenye Kitaburununu cha Maktaba ya Umma Jijini Iowa.

Nifanyeje ili Kupata Kadi ya Maktaba?

Wakazi wengi wa Iowa hupata Kadi ya Maktaba ya ICP kutoka katika Maktaba inayohamishika au katika tawi lililo jiji (Downtown Library). Jisajili binafsi ana kwa ajili ya kadi au mapema mtandaoni kwenye icpl.org/cards. Kitambulisho cha picha na uthibitisaji wa anwani ya mahali unakoishi vinahitajika.

Nifuate utaratibu upi kurudisha vitabu?

Unaweza kurudisha vitabu mahali popote ambapo Maktaba inayohamishika inasimama kwa wiki (angalia icpl.org/bookmobile upate ratiba ya msimu huu), katika kituo chochote cha nje, au Maktaba ya Umma ya Jijini Iowa.

Je, ninaweza kuchukua vitabu nilivyoshikilia au vinavyotoka katika maktaba nyingine katika Maktaba inayohamishika?

Naam, unaweza! Unapoomba kitu kishikiliwe au unapoazima kutoka maktaba nyingine, tafadhalii tujulishe kama ungependa kukichukua katika Maktaba inayohamishika.

Je, nitapata wapi ratiba mpya?

Unaweza kupata taarifa ya ratiba ya Maktaba inayohamishika katika icpl.org/bookmobile au kwa kuipigia Maktaba siku wakati wa saa za kazi. Huduma za Maktaba inayohamishika husimamishwa wakati kuna hali mbaya ya hewa au siku ambazo shule katika Jiji la Iowa zimefungwa kwa sababu ya hali ya hewa.



icpl.org/bookmobile

→ HAVE YOU heard the NEWS?

beginning JUNE 1,

there will be

NO FINES

on children's or

young adult

MATERIALS!

IOWA CITY
PUBLIC LIBRARY



See icpl.org/no-fines
for more information.



Sasa Maudhui ya Watoto na Vijana katika ICPL Hazitozwi Faini!

kuanzia tarehe 1 Juni 2019, maudhui yote ya Watoto na Vijana havitatozwa faini kwa kuecelewa.

Hii ina maana gani?

Kuna tofauti gani kati ya faini na ada ya kufidia?

Faini hutozwa kwa vitu ambavyo havijareshwa licha ya kupita kwa tarehe. Ada ya kufidia kwa ajili ya nyenzo za maktaba zilizopotea au zilizorejeshwa zikiwa zimeharibika. Bado utatakiwa kulipa ada ya kufidia vitu vilivyoharibika au ambavyo hujarejesha.

**Nina umru wa miaka 8, itakuwaje mamangu
akitungia kadi yangu kuchukua vitabu? Bado
nitatozwa faini akichelewa kurudisha kitabu
chake?**

Ndiyo. Faini ya kuchelewa hutozwa kwa nyenzo zote zilizochukuliwa na watu wazima bila kujali umri wa mwenye kadi. Nyenzo zilizo katika sehemu ya Watoto na Vijana ndivyo hazitozwo faini.

Je, nini kitafanyika nikisahau kurudisha kitu?

Ingawa mali ya maktaba iliyo katika sehemu ya Watoto na Vijana haitatozwa faini, ada ya kufidia itaanza kuhesabiwa kwa vitu visivyordishwa baada ya tarehe ya kurishwa kufika. Baada ya kitu husika kurudisha, ada ya kufidia itaondolewa.

**Je, bado nitakuwa nikikumbushwa kuhusu
kurudisha nyenzo?**

Kwa akaunti zilizo na anwani ya barua pepe inayofanya kazi, barua ya ukumbusho itatumwa siku mbili kabla ya tarehe ya kurudisha kufika. Baada ya tarehe ya kurudisha kufika, ukumbusho mmoja utatumwa. Vitu visivyorudishwa mara baada ya tarehe ya kurudisha kufika vitachukuliwa kuwa vimepotea na bili iliyo na ada ya kufidia itatumwa.



IOWA CITY
PUBLIC LIBRARY

123 S. Linn St. • Iowa City, IA 52240

319-356-5200 • icpl.org

HOURS: Mon-Thurs 10-9, Fri 10-8, Sat 10-6, Sun 12-5